# OFISI YA RAIS,

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

## SHULE YA MSINGI

## NUKUU ZA SOMO LA KISWAHILI

## DARASA LA TATU

MADAM RUTH LORMASS

# KUWASILIANA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

**Kutambua sauti mbalimbali**

**Irabu.**

a e i o u

**Konsonanti**

b c d f g h j k l m n p r s t v w y z.

**Silabi.**

Maana ya silabi

Silabi ni tamko au sauti ambayo huwa ni irabu au konsonanti na irabu

**Mfano:**

aaaa - irabu eeee - irabu iiii - irabu oooo - irabu

na - irabu na konsonanti li - irabu na konsonanti

nye - irabu na konsonanti ma - irabu na konsonanti

**Muundo wa silabi**

1. ba be bi bo bu
2. ma me mi mo mu
3. na ne ni no nu
4. da de do do du
5. ka ke ki ko ku

**Kuunda maneno**

1. pangoni
2. mwangwi
3. kitabu
4. wanafunzi
5. darasa

**Kutenganisha maneno**

1. Pa ngo ni ..............................................
2. mwa ngwi............................................
3. ki ta bu.................................................
4. wa na fu nzi...........................................
5. da ra sa..................................................

**Kuunda sentensi**

1. Bibi anasoma kitabu
2. Mama anapika wali
3. Kesho tutacheza mpira
4. Mwanafunzi anafundisha Kiswahili
5. Rafiki yake Neema ameumia

**Kutenganisha maneno yanayounda sentensi**

1. Bi bi a na so ma ki ta bu
2. Ma ma a na pi ka wa li
3. Ke sho tu ta che za mpi ra
4. Mwa li mu a na fu ndi sha ki swa hi li
5. Ra fi ki ya ke Ne e ma a me u mi a.

**Herufi mwambataono**

gh py nz sw lw ky tw nd sh th kw nyw shw ng'w.

**Kuweka irabu kwenye herufi mwambatano.**

1. gha
2. nzi
3. sha
4. twe
5. nda
6. nywe
7. thi

**Kuunda neno**

1. ghali
2. twende
3. nywele
4. shamba
5. swala
6. nzega
7. swaga

2. Neema na rafiki yake wanasoma shule gani?
   Neema na rafiki yake wanasoma shule ya msingi Mkwajuni

3. Nani alikuwa mwalimu wa zamu?
   Swaiba alikuwa mwalimu wa zamu.

4. Kwa nini wanafunzi wa darasa la tatu walikuwa na furaha?
   Wanafunzi wa darasa la tatu walikuwa na furaha sababu kila mwanafunzi alikuwa na hamu ya kuanza kusoma katika darasa jipya.

5. Je, unafikiri kwa nini ni muhimu kuwa na dada na kaka wa darasa.
   Ninafikiri ni muhimu kuwa na dada na kaka wa darasa kwa sababu waweze kutuongoza katika shughuli za darasani ikiwa ni pamaoja na kukusanya madaftari ya wanafunzi na kupeleka kwa mwalimu.

**ZOEZI LA 1.**

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino katika habari uliyosoma.
2. Unganisha sauti za herufi gh lw py nz sw tw na a e i o u kuunda silabi.

**Kwa mfano.**

Ukiunganiswa sauti ya herufi gh na sauti ya herufi a unaunda silabi gha.
a) gh a = gha
b) lw e = lwe
c) nz i = nzi
d) sw o = swo
e) tw u = twu

3. Tenganisha silabi zilizounda maneno yafuatayo kwa mfano:

a) wanafunzi - wa na fu nzi
b) walianza - wa li a nza
c) Jipya - Ji py a
d) anapaswa - a na pa swa

4. Tenganishwa sauti za herufi katika silabi zifuatazo. Kwa mfano:

a) Pya = py a
b) swa = sw a
c) nzu = nz u
d) ghi = gh i
e) lwa = lw a
f) twe = tw e

**ZOEZI LA 2.**

ghala ghorofa funza kwanza panzi

nzi kanzu kitanzi nzige swali

sweta swala mswaki jipya mpya

upya kilwa kulwa twanga tweta

twiga twisha patwa kutwa

**ZOEZI LA 3.**

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

1. Mwalimu amewauliza wanafunzi maswali
2. Baba amenunua nguo ya bei ghali
3. Wanafunzi wameanza kwenda shuleni
4. Huu ni mwaka mpya
5. Mjomba amejenga nyumba ya ghorofa
6. Kilwa ni mji mzuri
7. Kaka yake Kulwa anaitwa Mpetwa

ZOEZI LA 4.

Tunga sentensi mbili kwa kila neno lifuatalo pya ghali swali nzuri Kulwa

**SENTENSI.**

Mpya.

1. Siku ya sikukuu nilivaa nguo mpya
2. Mimi nimenunuliwa sare za shule mpya

Ghali

1. Peni hii nimenunua kwa bei ghali sana
2. Baba amenunua nyumba kwa bei ghali

Swali

1. Mwalimu ametupatia swali gumu sana
2. Mimi nilimuliza swali mwalimu

Nzuri.

1. Shule yetu ni nzuri sana
2. Peni yangu ni nzuri sana

Kulwa

1. Kulwa na Doto wamechelewa
2. Mimi ninaitwa Kulwa


Soma na andika maneno yenye sauti za herufi
ky pw ng’w nyw na shw py

Maneno:

1. ky - kwenye
2. pw - pwani, pweza,
3. ng’w - ng’wale
4. nyw - nywele

5. Shw - shwari
6. Py - mpya

Soma mazungumzo kati ya Sungura na Chui kisha fanya zoezi linalofuata.
Sungura: Habari za leo kaka Chui



Chui : Nzuri

Sungura : leo umekunywa maji?

Chui : sijanywa maji

Sungura : nataka nimuagize pweza atuletee maji kutoka baharini

Chui : Hapana. Kuna binadamu anaitwa Ng’wale anauza maji

Sungura : inaonekana humpendi pweza

Chui : si kweli. sina uadui na Pweza

Sungura : Nafikiri tuwaache wote tuagize maji kutoka kwa Kyando

Chui : Nakubaliana na wewe. Maji anayouza Kyando ni masafi sana

Sungura : Ni kweli itabidi tununue hayo

Chui : sawa mdogo wangu

ZOEZI LA 5

1. Tafuta maneno yenye suati za herufi ky pw ng’w na nyw katika mazungumzo uliyosoma.

Kwa mfano.

Ky - kyando

a) pw - pweza

b) ng’w - ng’wale

c) nyw - umekunywa, sijanywa

2. <u>Soma kwa sauti silabi zifuatazo</u>

Pwa kya ng’wa pwi nywa shwi
Kye shwa ng’wi kyo ng’we nywe

3.<u>Soma kwa sauti sentensi zifuatazo</u>

a) Bibi yangu anaishi Kyela

b) Baba anapenda kula pweza

c) Mzee Ng’wandu amejenga nyumba nzuri

Hali ya bahari ni shwari

ZOEZI LA 5.

Andika maana za maneno yafuatayo kwa kuchagua jibu sahihi.

Kwa mfano. Shwari - hali ya utulivu

| | |
|---|---|
| 1. shwari | kamba au uzi uliofungwa kwa duara |
| 2. ghali | yenye bei kubwa |
| 3. pweza | hali ya kutendeana ubaya baina ya watu |
| 4. kitanzi | mnyama wa baharini |
| 5. uadui | hali ya utulivu |

MAJIBU.

1. shawari - hali ya utulivu
2. ghali - yenye bei kubwa
3. pweaza - mnyama wa baharini
4. kitanzi - <u>kamba au uzi uliofungwa kwa duara</u>
5. uadui - <u>hali ya kutendeana ubaya baina ya watu</u>

<u>JIULIZE.</u>

Umejifunza nini katika sura hii?

Katika sura hii nimejifunza,

1. <u>Irabu</u>
2. <u>Konsonanti</u>
3. <u>Silabi</u>
4. <u>Kuunda maneno</u>
5. <u>Kutenganisha maneno</u>
6. <u>Herufi mwambatano</u>
7. <u>Kuunda sentensi</u>
8. <u>Kutenganisha maneno yanayounda sentensi</u>
9. <u>Kuunganisha sauti na herufi</u>


**KUTUMIA MATAMSHI SAHIHI KATIKA KUTAMKA MANENO.**

Kutamka maneno yenye sauti za herufi s na th, za na dh, l na r, g na


Kutamka maneno yenye sauti za herufi s na


**Tazama picha zifuatazo kisha fanya zoezi linalofuata.**














ZOEZI LA 1

1. **Kutamka majina ya vitu ninavyoviona katika picha namba 1 hadi 5.**
   1. Pasi
   2. Msumari

3. Sabuni
4. Fenesi
5. Samaki

2. **2. Kutamka kwa sauti namba ninazoziona katika picha namba 6 na 7.**
   6. Themanini
   7. Thelathini

3. **Taja sauti za mwanzo inayosikika katika kutamka maneno. Samaki, sabuni, sarafu, na saa.**
   Samaki - s Sabuni - s Sarafu - s Saa - s

4. **Kutaja suati ya mwanzo inayosikika katika kutamka namba 80 na 30.**
   80 - th
   30 - th

ZOEZI LA 2.
Soma maneno yafuatayo kwa sauti.


saa sabuni subiri soko safari sahani saruji msumari usafi pasi fenesi msusi thelathini themanini thamani thubutu theluji urithi.


ZOEZI LA 3.
Nakili sentensi zifuatazo katika daftari lako kisha chagua neno sahihi kwa kupigia mstari. Kwa mfano:
(samaki, thamaki) ni chakula bora.

1. Baba anavua (thamaki, samaki)
2. Mimi ninaoga kwa kutumia maji safi na (sabuni, thabuni)
3. Juma anaishi karibu na (thoko, soko)
4. Mwanafunzi mtiifu amepata alama (semanini, themanini)
5. Mimi ninapenda kula (fenesi, fenethi)

Kutamka maneno yenye sauti za herufi za na

Tazama picha zifuatazo kisha fanya zoezi linalofuata.





ZOEZI LA 4.

1. Kutamka majina ya vitu ninavyoviona katika picha namba 1 na 2.
    a) Zabibu
    b) Zeze

2. Kutaja sauti ya mwanzo inaosikika katika kutamka maneno yafuatayo.
    a. zawadi - z

    zulia - z

    zahanati - z

    zeze – z

    zao - z

    zabibu - z

    b. dharau - dh

    dhaifu - dh

    dhoofu - dh

    dhoruba - dh

ZOEZI LA 5.

Soma maneno yafuatayo kwa sauti.

ziwa mnazi mzazi maziwa

zito zamani mzazi maziwa
dharura madhara dhahabu
adhabu dhuluma dhoruba dharau zuia
dhoofu dhambi dhuru nazi

ZOEZI LA 6.

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchagua neno sahihi.
Kwa mfano:
Dhahabu hupatikana Tanzania (Zahabu, dhahabu)

1. Mimi ninapenda kupiga zeze (dheze, zeze)
2. Gunia lililojaa viazi ni zito. (dhito, zito)
3. Pamba ni zao la biashara. (zao, dhao)
4. Mama alisema kuwa kuiba ni dhambi (dhambi, zambi)
5. Juma alikwenda kuwatembelea wazazi wake (wadhazi, wazazi)

Kutambua maneno yenye sauti za herufi l na r.





ZOEZI LA 7.


Soma maneno yafutayo kwa sauti.

ladha lazima linda lala lami elea

lima mali liza alika koroboi
barabara ridhia redio rika jeraha
raba robo rudi bure roho ruhusa riadha.

ZOEZI LA 8.
Tazama picha zifuatazo kisha tunga sentensi mbili kwa kila picha. Mfano:



1. Huu ni mlango

2. Nyumba yetu ina mlango mzuri.

SENTENSI.
1. Hii ni rula
2. Mimi nina rula ndefu

1. Hii ni peni

2. Peni hii amenipa baba

1. Huyu ni baba
2. Baba analima shambani

1. Hiki ni kiberit
2. Njiti za kiberiti ni nene sana

1. Hii ni redio
2. Bibi anasikiliza redio

ZOEZI LA 9.

1. Andika kisha soma maneno yafuatayo kwa usahihi. Mfano:

zulia - zuri

a. bule - bure
b. rami - lami
c. luhusa - ruhusa
d. loho - roho
e. ria - lia
f. ledio – redio
g. balabala – barabara
h. jelaha - jeraha

ZOEZI LA 10.

**Soma maneno yafuatayo kwa sauti.**

gari gauni ugali fagio gego gitaa goti gunia guta ghali ghala lugha ghorofa gharama.

ZOEZI LA 11.

Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kw kutumia herufi g au gh kisha soma maneno hayo kwa sauti.

1. gari - _ari
2. gunia - _unia
3. ugua - u_ua
4. goti - _oti
5. ghali - _ali
6. gogo - _ogo
7. ghala - _ala
8. gitaa - _itaa
9. lugha - lu_a
10. gharama - _arama
11. ghasia - _asia
12. ghorofa - _orofa

ZOEZI LA 12.

1. Nakili chati ya maneno ifuatayo katika daftari lako kisha weka alama ya (v) kwa neno sahihi na (x) kwa neno lisilo sahihi.

| | | |
|---|---|---|
| Samaki V | zawadi V | saruji V |
| thoko X | Ziwa V | sabuni V |
| gorofa X | Dhambi V | ruka V |
| dhuluma V | thamaki X | ulithi X |
| dhiwa X | Subiri V | |
| gati X | sukari V | |
| ledio X | lugha V | |
| rara X | luhusa X | |

2. Kuorodhesha maneno yote yasiyo sahihi kutoka katika chati ya swali la kwanza na uyaandike kwa usahihi.


3. Kwa mfano.
    a) Ledio - redio
    b) thoko - soko
    c) gorofa - ghorofa
    d) thamaki - samaki
    e) ulithi - urithi
    f) dhiwa – ziwa
    g) gali - gari
    h) rara - lala
    i) luhusa - ruhusa


JIULIZE.


Kuna umuhimu gani wa kutamka maneno kwa usahihi? Umuhimu wa kutamka maneno kwa usahihi ni ..........................................................................................


Kuanzisha na kuendeleza vitu mbalimbali katika umoja na wingi.


Tazama picha zifuatazo kisha fanya zoezi linalofuata.































ZOEZI LA 1.

1. Vitu vinavyoonekana katika picha namba 1 hadi 6 vinapatikana

a) Shuleni

b) Nyumbani

c) Sokoni

d) Dukani

2. Kutaja majina ya vitu hivyo katika hali ya umoja na wingi. Kwa mfano:

Kiti - viti

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kiti | Viti |
| Daftari | Madaftari |
| Kijiko | Vijiko |
| Mpira | Mipira |

| | |
|---|---|
| Chungwa | Machungwa |

<u>KIFAA</u> <u>MATUMIZI</u>

Kiti <u>Kukalia</u>
Daftari <u>Kuandikia</u>
Mti <u>Kupumzika, kuni, mkaa, mbao</u>
Kijiko <u>Kulia na kupakulia chakula</u>
Mpira <u>Kuchezea</u>

<u>ZOEZI LA 2</u>.

1. Kutaja vitu vingine vitano vinavyopatikana shuleni.

a) <u>Dawati</u>

b) <u>Jembe</u>

c) <u>Meza</u>

d) <u>Penseli</u>

e) <u>Peni</u>

2. Kutaja majina ya vitu hivyo katika hali ya umoja na wingi.

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Dawati | Madawati |
| Jembe | Majembe |
| Meza | Meza |
| Penseli | Penseli |
| Peni | Peni |

3. Kueleza matumizi ya kila kimoja

<u>Kwa mfano</u>: Kiti hutumika kukalia

<u>KIFAA</u> <u>MATUMIZI</u>

Dawati <u>kukalia</u>

Jembe <u>kulimia</u>

Meza <u>kuwekea vitu wakati unaandika au kula</u>

Penseli <u>kuandika na kuchorea</u>

Peni <u>kuandika</u>

<u>ZOEZI LA 3.</u>

1. Kutaja wingi wa vitu vifuatavyo.

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Gari | Magari |
| Sufuria | Masufuria |
| Mchanga | Mchanga |
| Simu | Simu |

| | |
|---|---|
| Chupa | Vyupa |
| Jiwe | Mawe |
| Jembe | Majembe |
| Koti | Makoti |
| Nyumba | Nyumba |
| Mti | Miti |
| Shati | Mashati |
| Nywele | Nywele |
| Wembe | Nyembe |
| Gauni | Magauni |
| Taa | Taa |

2. Kutaja umoja wa vitu vifuatavyo:





| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Yai | Mayai |
| Embe | Maembe |
| Maji | Maji |
| Mti | Miti |
| Mguu | Miguu |
| Unga | Unga |
| Mfuko | Mifuko |
| Jicho | Macho |
| Maziwa | Maziwa |
| Begi | Mabega |
| Ini | Maini |
| Kidole | Vidole |



Kubadili sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya wingi. <u>Kwa mfano:</u>
Rangi hii ni nzuri <u>Rangi hizi ni nzuri</u>

1. Mfuko huu ni mkubwa: <u>Mifuko hii ni mikubwa</u>
2. Meza hii ni safi: Meza hizi ni safi
3. Nyumba hii ni nzuri: Nyumba hizi ni nzuri
4. Kitabu hiki ni kidogo: Vitabu hivi ni vidogo
5. Jiwe hili ni kubwa: Mawe haya ni makubwa
6. Miti mirefu imeanguka: <u>Mti mrefu umeanguka</u>
7. Baba amenunua magari mawili: Mwanafunzi amenunua gari moja
8. Wanafunzi wamepanda maua mazuri: Mwanafunzi amepanda ua zuri
9. Madarasa yetu yana madirisha makubwa: Darasa letu lina dirisha kubwa
10. Taa za shule yetu zinawaka vizuri: <u>Taa ya shule yetu inawaka vizuri</u>.

**<u>Kutambua methali katika mazungumzo .</u>**

Soma na igiza mazungumzo yafuatayo wewe na mwenzako.

| | |
|---|---|
|  | Mimi ni Swala. Najua kukamilisha methali hii. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Nina akili kuliko wanyama |
|  | Mimi ni Twiga. Ni mwerevu zaidi kuliko swala. Ninajua maana ya hiyo methali. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Maana yake, asiyesikia anayoambiwa na wakubwa hupata matatizo. Ninawashinda wanyama wote kwa akili. |
|  | Mimi ni Simba. Ninajua kukamilisha methali, methali hiyo ni Ahadi ni deni. Mimi ni shujaa kuliko wanyama wote. |
|  | Mimi ni Sungura. Ni mjanja kuliko simba. Ninajua maana ya methali; ahadi ni deni, maana yake ukiahidi jambo ulitekeleze. Mimi ni hodari kuliko wanyama wote. |

| | |
|---|---|
| | |
|  | Mimi ni Nyati. Ninajua kukamilisha methali tofauti na zilizotajwa. Haba na haba ujaza kibaba. Mimi ni makini kuliko wanyama wote. |
|  | Mimi ni Tembo, ninajua maana ya hiyo methali, haba na haba hujaza kibaba, maana yake kidokidogo mwishowe huongezeka. Mimi ni mkubwa na mwenye uwezo kuliko wanyama wote. |

ZOEZI LA 6.

Kumalizia methali zifuatazo kwa kuchagua jibu sahihi.

| hajikwai haiozi, yaumiza matumbo, hula mbivu arobaini, haina baraka si ujinga |
|---|

Kwa mfano:

Ngoja ngoja yaumiza matumbo.

1. Mvumilivu hula mbivu
2. Kuuliza si ujinga
3. Mwenda pole hajikwai
4. Siku za mwizi ni arobaini
5. Akiba haiozi
6. Haraka haraka haina baraka

NAHAU.

Kueleza maana ya nahau zifuatazo.

| | |
|---|---|
| 1. Nahau:<br>Maana : | Kufa kishujaa<br>Kushindwa baada ya kujitahidi sana |
| 2. Nahau:<br>Maana: | Piga marufuku<br>Kataza |
| 3. Nahau:<br>Maana: | Kula kiapo<br>Toa ahadi, apa |

| | |
|---|---|
| 4. Nahau:<br>Maana: | Meza mate<br>Tamani kitu |
| 5. Nahau:<br>Maana | Kitinda mimba<br>Mtoto wa mwisho kuzaliwa |

Kutumia nahau katika sentensi.

1. Kufa kishujaa.

   Askari wetu wamekufa kishujaa vitani

2. Piga marufuku

   Mama alipiga marufuku kurudi usiku.

3. Kula kiapo

4. Hadithi hiyo ilikuwa na mafunzo gani?

   Hadithi hiyo ilikuwa na mfunzo ya tusimuamini kila mtu na tuwe a huruma.

ZOEZI LA 7.

1. Sikiliza hadithi itakayosimuliwa na mwalimu.

Amina anaishi na bibi yake katika kijiji cha Mawenzi. Anamsaidia bibi yake shughuli za nyumbani. Shughuli hizo ni kama vile kusafisha nyumba. Leo Amina alimuliza bibi yake, bibi unajua kusoma? Bibi akamjibu ndiyo ninajua kusoma na kuandika. Amina akamwambia bibi, sawa bibi kesho nitaleta kitabu change ili tusome pamoja.

2. Kusimulia hadithi hiyo kwa maneno yangu mwenyewe.

Amina na bibi yake wapo katika kijiji cha Mawenzi. Amina huwa anapenda kumsaidia bibi yake kazi za nyumbani. Kazi hizo ni kufua, kupika, kuosha vyombo, na kusafisha nyumba. Jama Amina alimuliza bibi, anajua kusoma? Bibi akamwambia ninajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Amina akamueleza bibi yake , kesho nitakuja na kitabu ili unisomee, kisha tosome sote.

3. Hadithi hiyo inatufundisha nini?

Hadithi hiyo inatufundisha

a) Tusaidie kazi
b) Tusiwe wavivu
c) Tupendane

ZOEZI LA 8.


1. Angalia picha hizi kisha andika hadithi fupi.














Siku moja bibi alimtuma mjukuu wake kwenda gengeni kununua nyanya. Alipokuwa anarudi alikutana na rafiki yake. Wakaanza kucheza mpira. Huku wakati wanacheza nyanya zikamwagika. Mama mmoja akawaona na kuanza kumgombeza mjukuu wa bibi na kumwambia aziokote nyanya, na Yule mama akampeleka mjukuu hadi kwa bibi yake. Bibi alimgombeza mjukuu wake.

2. Soma hadithi uliyoandika kwa sauti.
3. Hadithi uliyoandika inatufundisha nini?
   Hadithi niliyoandika inatufundisha tukitumwa tusicheze njiani.

JIULIZE.

Kuna umuhimu gani wa kusimulia au kusikiliza hadithi? Umuhimu wa kusimulia au kusikiliza hadithi ni:-

a) Inaburudisha
b) Inaliwaza
c) Inaelimisha
d) Tunajifunza mambo mbalimbali

Kutoa taarifa kuhusu tukio lililotokea

1. Taarifa ni habari inayotolewa ili kujumlisha jamii jambo Fulani.
2. Vyombo vinavyotoa taarifa.

a) Magazeti
b) Simu
c) Runinga
d) Intaneti
e) Barua

Ajali za barabarani

1. Ajali ya gari
2. Ajali ya baiskeli
3. Ajali ya pikipiki
4. Ajali ya bajaji
5. Ajali ya treni

Kueleza tukio la ajali

Ajali ya pikipiki.

Mdogo wangu alitumwa na mama dukani, kununua mchele. Wakati anavuka barabara aligongwa na pikipiki na mguu wa kulia ukavunjika. Tulimpeleka hospitalini akapatiwa matibabu. Na sasa anaendelea vizuri.

Mambo yanayosabisha ajali.

1. Ulevi
2. Mwendokasi
3. Kutofahamu sheria za barabarani
4. Kusinzia
5. Ubovu wa miundo mbinu
6. Ubovu wa vyombo vya usafiri
7. Hali ya hewa (mfano ukungu)
8. Kutokuwa na taaluma kwa watu wanaoendesha vyombo vya usafiri

Madhara ya ajali.

1. Kifo
2. Ulemavu wa kudumu
3. Hasara
4. Taifa kupoteza wataalamu
5. Jamii kupoteza wategemezi
6. Familia kayumba kimaisha
7. Kuongezeka kwa idadi ya wategemezi
8. Kuongezeka kwa ombaomba
9. Kuongezeka kwa idadi ya watoto wa mitaani

Majina ya wanafamilia (uk. 67)

1. Asha
2. Yusta
3. Wiliamu
4. Hawa
5. Mwajuma
6. Joni

UHUSIANO.

1. Asha - Mama
2. Yusta - Dada
3. Wiliamu - Mjomba
4. Hawa - Shangazi
5. Mwajuma - Bibi

6. Joni - baba.

UHUSIANO WA WATU KATIKA FAMILIA.
Soma habari hii
Familia ya Chalo.

Mimi ninaitwa Chalo. Baba yangu anaitwa Daudi na mama yangu anaitwa Nakiete. Kaka yangu anaitwa Tumaini na dada yangu anaitwa Sofia. Bibi anaitwa Chakole na babu anaitwa Kalonga. Mimi ni mjukuu wao. Baba ana mdogo wake anayeitwa Kimoso. Mama ana dada yake anayeitwa Jema. Jana mjomba Jako alikuja kutusalimia. Leo asubuhi shangazi Sara amekuja kutusalimia. Amekuja na mtoto wake anayeitwa Kandida. Kandida ni binamu yangu. Mimi na Kandida tunacheza pamoja.



ZOEZI LA 1.

Jibu maswali ya kutambua uhusiano wa wanafamilia ya Chalo.

a. Tumaini anamwita Sofia dada
b. Tumaini anamwita Kalonga babu
c. Sofia anamwita Jako mjomba
d. Tumaini anamwita Chakole bibi
e. Kandida anamwita Chalo binamu
f. Sofia anamwita Sara binamu
g. Sofia anamwita Jema shangazi
h. Kimoso anamwita Daudi Kaka

i. Sofia anamwita Kimoso baba mdogo

ZOEZI LA 2.

1. Taja majina ya watu katika familiya yako.

Kwa mfano:

Mjomba wangu anaitwa Msoke.

1. Kaka yangu anaitwa Musa
2. Bibi yangu anaitwa Nkoma
3. Baba yangu anaitwa Joni
4. Shangazi yangu anaitwa Mwajuma
5. Mama yangu anaitwa Sara

ZOEZI LA 3.

Kamilisha sentensi za kifungu A kwa kuchagua neno sahihi kutoka kifungu B.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| 1. Baba wa baba yako unamwita<br>2. Mzazi wako wa kike unamwita<br>3. Mtoto wa mjomba wako unamwita<br>4. Mkubwa wako wa kike unamwita<br>5. Kaka wa mama yako unamwita<br>6. Mzazi wako wa kiume unamwita<br>7. Mdogo wa kike wa mama yako unamwita<br>8. Kaka yake baba yako unamwita<br>9. Ndugu yako mkubwa wa kiume unamwita<br>10. Mama wa baba yako unamwita<br>11. Baba wa mama yako unamwita | A. Baba<br>B. Kaka<br>C. Shangazi<br>D. Mama mdogo<br>E. Mjomba<br>F. Bibi<br>G. Shemeji<br>H. Binamu<br>I. Mama<br>J. Wifi<br>K. Babu<br>L. Baba mkubwa<br>M. Dada<br>H. Mjukuu |


MAJIBU.

1. Dada wa baba yako unamwita shangazi
2. Mzazi wako wa kike unamwita mama
3. Mtoto wa mjomba wako unamwita binamu
4. Mkubwa wako wa kike unamwita dada
5. Kaka wa mama yako unamwita mjomba
6. Mzazi wako wa kiume unamwita baba
7. Mdogo wa kike wa mama yako unamwita mama mdogo
8. Kaka yake baba yako unamwita baba mkubwa
9. Ndugu yako mkubwa wa kiume unamwita kaka
10. Mama wa baba yako unamwita bibi
11. Baba wa mama yako unamwita babu.

ZOEZI LA 4.

1. Kuchora picha za watu wanne wa familia yangu.
2. Chini ya kila picha kuandika jina la uhusiano


Mfano. baba, mama, kaka na dada



BA
BA



MA
MA



KA
KA



DA
DA

ZOEZI LA 5.

IMLA.

Sikiliza babari atakayokusomea mwalimu kisha uandike.

1. Bibi alitusimulia hadithi
2. Asha anasoma darasa la tatu
3. Babu anaishi Sengerema
4. Mama jana alinunua samaki
5. Mwamvuli wa dada umevunjika.



JIULIZE.
Kuna faida gani za kujifunza uhusiano wa watu katika familia.
Faida za kujifunza uhusiano wa watu katika familia ni kujua jinsi ya uhusiano ulivyo katika familia na jinsi ya kuitana.
MAJINA YA WANYAMA NA WADUDU.



Kujibu maswali ya wanyama wafugwao





1. Kutaja majina ya wanyama wafugwao.
   a) Paka
   b) Mbwa
   c) Ng'ombe
   d) Mbuzi
   e) Kondoo
2. Kutaja majina ya wanyama wa porini.
   a) Fisi
   b) Simba
   c) Chui
   d) Pundamilia
   e) Swala
   f) Tembo
   g) Nyani
3. Wanyama wa porini niliowahi kuwaona ni :-
   a) Pundamilia
   b) Swala
   c) Tembo
   d) Nyani
   e)
4. Ndiyo. Ninapenda kufuga wanyama. Kwa sababu wanavutia na wanapendana sana.

ZOEZI LA 1.

1. Kutaja majina ya wanyama wafuatao.

2. Soma na fumbua mafumbo yafuatayo.

**Mimi ni nani?**

a) Ninakupatia nyama, maziwa na pesa. Ngozi yangu hutumika kutengenezea ngoma na mikanda. Ninatoa sauti moooo! Je, mimi ni nani?
Jibu: ng’ombe.

b) Ninakupatia nyama, manyoya yangu hutumika kutengenezea nguo. Mkia wangu umejaa mafuta. Ninalia baaa! Je, mimii ni nani?
Jibu: mimi ni kondoo.

c) Ni mkubwa kuliko wanyama wote porini. Nina mkonga mrefu na masikio makubwa. Watalii husafiri kuja kuniona. Je, mimi ni nani?
Jibu: mimi ni tembo.

d) Ni rafiki wa binadamu. Ni mkali, nalinda nyumba na ninafukuza wezi. Ninabweka, wu, wu, wu, wu! Je, mimi ni nani?
Jibu: mbwa.

e) Ni rafiki wa binadamu. Ni mpole, ninapenda kukaa jikonI. Ninapenda kula samaki na kunywa maziwa. Ninamwiwinda panya. Je, mimi ni nani?
Jibu: Paka

f) Nina shingo ndefu kuliko wanyama wote wa porini. Ninakula majani ya juu ya mti. Ninatembea kwa maringo. Ni kivutio cha watalii. Picha yangu katika noti ya Tanzania. je, mimi ni nani? .
Jibu: Twiga

g) Ninaishi porini. Ngozi yangu ina mistari myeupe na myeusi. Watu hufurahi wanaponitazama. Je, mimi ni nani
Jibu: pundamilia.

h) Ninaishi majini, kwenye mito, maziwa na nchi kavu. Nina mdomo mpana meno makali, ngozi yangu hutumika kutengenezea mapambo. Ninafanana na kenge ingawa nimemzidi ukubwa. Je, mimi ni nani?
Jibu: jibu ni mamba.

i) Ninaishi kwenye miti porini. Ninakula mazao ya binadamu. Nina tabia ya kurukia miti. Nina mkia mrefu. Je, mimi ni nani?
Jibu: ngedere.

j) Ninaishi porini. Ninapenda kula mizoga. Je, mimi ni nani?
Jibu: fisi.

ZOEZI LA 2.

Igiza mafumbo ya mimi ni nani? Katika zoezi la 1.

ZOEZI LA 3

1. Kutaja wanyama watano ninaowafahamu. Kwa kila mnyama kueleza muonekano na sifa zake.

a. Twiga.
Muonekano.
- Ana madoa madoa
- Ana shingo ndefu
- Sura ndefu

Sifa.
- Anavutia watalii

- Anatembea kwa maringo
- Anakula majani juu kabisa
- Anaonekana kwenye noti ya Tanzania (picha)

b. Mamba.

Muonekano.

- Anafanana na kenge
- Ana umbo kubwa

Sifa.

- Meno yake ni makali
- Ana mdomo mkubwa
- Ngozi hutengenezea mapambo

c. Ng'ombe.

Moenekano.

- Ana umbo kubwa
- Ana pembe

Sifa:

- Ngozi hutumika kutengenezea ngoma na mikanda
- Hutupatia, nyama, maziwa na pesa.

d. Ngedere

Muonekano.

- Ana umbo dogo
- Mkia mrefu

Sifa:

- Anakula mazao ya binadamu
- Hurukia miti
- Ana mkia mrefu

e. Tembo


Muonekano.

- Ana umbo kubwa
- Masikio makubwa


Sifa:

- Ana mkonga mrefu
- Huvutia watalii

2. Kuchora picha ya mnyama wa porini.



3. Kuchora picha ya mnyama anayefugwa



<u>Sifa na tabia za wadudu.</u>

<u>Kujibu maswali yafuatayo.</u>

1. Kutaja majina ya wadudu watatu ninaowafahamu.
    a. Jongoo
    b. Tandu
    c. Mende
2. Wadudu hao wanatofautiana kwa mambo ya:
    a) Jongoo
        i. Ana miguu mingi
        ii. Ngozi yake imekatika katikakatika mfano wa pete
        iii. Anajikunja anakuwa kama O
        iv. Akinyooka anakuwa kama namba moja
    b) Tandu.
        i. Anang’ata
        ii. Ana miguu mingi
        iii. Mkia wake umegawanyika
    c) Mende.
        i. Ana mabawa mawili
        ii. Ana miguu minne
        iii. Ana pembe ndefu
        iv. Anaruka
        v. Anakaa sehemu chafu kama chooni
3. Wadudu wanaopatikana katika mazingira ya nyumbani ni :-
    a) <u>Inzi</u>
    b) Mende

c) Kipepeo
d) Tandu
e) Jongoo
f) Nyuki
g) Nge

4. Kueleza tabia za wadudu niliowataja.
   a) Nzi

- Anapenda kukaa chooni
- Anapenda kula vitu vichafu
- Anaeneza magonjwa
- Anaruka

b) Mende

- Ana mabawa mawili
- Anaruka
- Ana pembe ndefu
- Anakaa sehemu chafu

c) <u>Kipepeo</u>

- Anaruka

d) <u>Tandu</u>

- Anang'ata

e) <u>Jongoo</u>

- Akijikunja ankuwa kama O
- Akinyooka anakuwa kama namba moja

<u>f) Nyuki</u>

- Anang'ata
- Anatengeneza asali
- Anabeba maua

<u>g) Nge.</u>

- Anang'ata kwa kutumia mkia
- Wakati wa kutembea mkia ananyanyua juu


5. Kutaja wadudu wawili na madhara yake wanayoleta kwa binadamu.
   a) Nzi
   - Anaeneza magonjwa

   b) <u>Nyuki.</u>

   - Anang'ata.

<u>ZOEZI LA 4.</u>

Kuchora picha zifuatazo kisha jibu maswali.



MASWALI

1. **Kutaja majina ya wadudu wanaonekana katika picha.**
   a) Kipepeo
   b) Mende
   c) Nge
   d) Nzi
   e) Nyuki
   f) Jongoo
   g) Panzi
   h) Buibui
   i) Dondola
   j) Tandu
   k) Kaa
2. **Kutaja wadudu wanaoruka**
   a) Mende
   b) Kipepeo
   c) Nzi
   d) Dondola
   e) Nyuki
3. **Kutaja tabia za wadudu hao**

   Mende.
   - Anaruka
   - Anakaa sehemu chafu

   Nzi
   - Anaruka
   - Anakaa sehemu chafu
   - Anaeneza magonjwa

   Nyuki
   - Anaruka
   - Anang'ata
   - Anakusanya maua kwa ajili ya kutengeneza asali

   Kipepeo.
   - Anaruka

   Dondola
   - Anaruka
   - Anang'ata
4. **Kutaja wadudu wanaotambaa**
   - Jongoo
   - Tandu
   - Nge

- Kaa

5. **Kuelezea tabia za wadudu hao.**

Jongoo.
- Anajikunja anakuwa kama O
- Akinyooka anakuwa kama namba moja
- Anatambaa

Tandu
- Anang’ata
- Anaruka

Nge
- Anang’ata

Kaa
- Ukimchokoza anajikunja
- Ana uwezo wa kuchimba shimo
- Anaweza kukaa chini ya shimo.



Soma habari kisha jibu maswali

Daudi ang’atwa na nyuki.

MASWALI.

1. Daudi aliona wadudu gani porini?

   Daudi aliona nyigu, panzi na siafu porini.
2. Ni wadudu gani hatari kati ya wadudu aliowaona Daud

   Nyigu na siafu ni wadudu hatari kati ya wadudu aliowa
3. Kwa nini Daudi aling’atwa na nyuki?

   Daudi aling’atwa na nyuki kwa sababu aliwapiga.
4. Kama ungeng’atwa na nyuki kama Daudi ungefanya ni

   Kama ningeng’atwa na nyuki kama Daudi ningeenda h
5. Nyuki wana faida gani?

   Nyuki wana faida ya kutupatia asali, na fedha.
6. Habari hii inatufundisha nini?

Habari hii inatufundisha

a. Tusiwapige au kuwachokoza wadudu


b. Tusipende kutembea peke yetu porini

ZOEZI LA 5.

Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kutumia picha.

1. Ukoo wetu hauishiwi na safari.
   Jibu: siafu.
2. Kafa huku akining’inia
   Jibu: buibui

3. Mwanangu hunipa kitu kitamu lakini akichokozwa hutawanya watu.
   Jibu: nyuki
4. Ana miguu ya msumeno
   Jibu: Panzi
5. Akijikunja anakuwa herufi O akijinyoosha anakuwa namba moja.
   Jibu: jongoo
6. Na mdomo lakini anang’ata kwa mkia.
   Jibu: nge



JIULIZE

Kujua sifa na tabia za wanyama na wadudu zitakusaidiaje katika maisha yako?

Kujua sifa na tabia za wanyama na wadudu zitakusaidia kujua wanyama na wadudu wepi ni hatari kwangu na kujihadhari nao. Pia itanisaidia wanyama na wadudu wepi ni rafiki (hawana madhara) kwa binadamu.

KUANDIKA HABARI KUZINGATIA TARATIBU ZA ALAMA ZA UANDISHI UK. 27.

Alama za uandishi

1. Nukta au kituo .
2. Mkato ,
3. Mshangao !

Ulizo ?

Funga na fungua semi “ ”

Kutumia alama . ! ?na “ ” katika sentensi.

Kujibu maswali haya.

1. Kutaja majina ya alama hizi. . , ! ? “ ”
   . nukta/kituo
   ‘ mkato


! mshangao
? ulizo
“ ” Funga na fungua semi.


2. 2. Alama , inatumika wapi?


   Alama , inatumika kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa kwa mfululuzo. Kwa mfano:
   Chumvi, sukari, mkate, maharage.

Angalia picha kisha soma sentensi kwa sauti. Chunguza matumizi ya alama katika sentensi hizo.













ZOEZI LA 1.


1. **Kutaja alama za uandishi ninazoziona katika sehemu ya 1 hadi 5.**


a) Sentensi ya kwanza imetumia kituo
b) Sentensi ya pili imetumia ulizo
c) Sentensi ya tatu imetumia mkato na funga na fungua semi.
d) Sentensi ya nne imetumia mshangao na nukta.
e) Sentensi ya tano imetumia mkato na nukta.



2. **Alama ya kituo hutumika mwishoni mwa sentensi.**

ZOEZI LA 2.

Soma na igiza.

| | |
|---|---|
|  | Mimi ni nukta, kwa jina lingine ni kituo kikubwa. Hutumika mwishoni mwa sentensi. Alama yangu ni hii**.** |
|  | Mimi ni mkato, watu wengi huniita kituo kidogo. Hutumika kutenganisha vitu vilivyoorodheshwa kwa mfulululizo. Alama yangu ni hii **,** |
|  | Mimi ni mshangangao! Watu hunitumia kila wanaposhangaa, alama yangu ni hii **!** |

| | |
|---|---|
|  | Mimi ni ulizo, hutumika kila linapoulizwa swali. Alama |

| | |
|---|---|
|  | Mimi ni funga na fungua semi. Hutumika katika maneno halisi ya mzungumzaji. Alama yangu ni hii “ ” |
|  | Mimi ni herufi kubwa. Watu hunitumia sana mwazoni mwa majina yao. Pia hunitumia mwanzoni mwa majina ya miji au majina ya mahali. Mimi nina sura ya kila herufi. Baadhi ya herufi hizo ni A B C D E F. |

<u>ZOEZI LA 2.</u>

Weka alama . , “ ” ana ! kwa usahihi mbele ya jina la alama. Kwa mfano.
Kituo kikubwa .

| JINA | **ALAMA** |
|---|---|
| Mkato | , |
| Mshangao | ! |
| Ulizo | ? |
| Funga na fungua semi | “ ” |
| Kituo kikubwa | . |

ZOEZI LA 3.
Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi kwa kuweka alama za uandishi na herufi kubwa.

1. Sebo anaishi mkoa wa Morogoro
   Sebo anaishi mkoa wa Morogoro
2. Wanafunzi walitembelea mbuga za wanyama za mikumi, Serengeti na Ngorongoro.
   Wanafunzi walitembelea Mbuga za wanyama Mikumi, Serengeti na Ngorongoro.
3. Lo mtoto ameanguka
   Lo! Mtoto ameanguka.
4. Shambani kwenu kuna mazao gani.
   Shambani kwenu kuna mazao gani?
5. Bibi alisema karibu mjukuuu wangu.
   Bibi alisema, karibu mjukuu wangu.

**Soma habari hii kisha jibu maswali.**

**KITUO CHA AFYA.**

Mimi ninaitwa Luka. Kaka yangu anaitwa Kizenga. Tunaishi katika kijiji cha Kwale. Katika kijiji chetu kuna kituo cha afya. Siku moja niliugua mafua makali na kikohozi. Baba akaniuliza "umeanza lini kukohoa?" "nikamjibu Nilianza kukohoa tangu jana jioni. "Baba akamwambia kaka, "Kizenga mpeleke Luka kwenye kituo cha afya akatibiwe". Kaka aliponiona alishangaa akasema "Lo! Kumbe unaumwa sana? Pole sana mdogo wangu. Twende kwenye kituo cha afya ukatibiwe.

Tulipofika kwenye kituo cha afya tuliwakuta wagonjwa wengi. Baada ya muda, mwuguzi alituita na katika chumba cha daktari. Mimi na kaka tuliingia kwa daktari. Tulipofika kwa daktari, nilimueleza jinsi ninavyoumwa. Daktari akaniuliza, "ulianza lini kukohoa?" nikamjibu, nilianza kukohoa jana jioni." Daktari akanipima kisha akaniandikia dawa. Baada ya kupata matibabu mimi na kaka tulirudi nyumbani.



MASWALI.

1. Taja alama za uandishi zilizojitokeza katika habari hii. Alama za uandishi zilizojitokeza katika habari hii ni
   a) Nukta/kituo kikubwa
   b) Mkato
   c) Funga na funga semi
   d) Mshangao
   e) Ulizo
2. Ni alama gani za uandishi zimejitokeza mara nyingi zaidi? Alama zilizojitokeza mara nyingi zaidi ni:-
   a) Nukta /kituo kikubwa
   b) Funga na fungua semi
   c) Mkato
3. Alama gani zimejitokeza kwa uchache? Alama zilizojitokeza kwa uchache ni
   a) Ulizo
   b) Mshangao
4. Je, herufi kubwa imetumika wapi? Herufi kubwa imetumika
   a) Mwanzoni mwa neno
   b) Mwanzoni mwa majina

ZOEZI LA 4.
Rudia kusoma habari ya kituo cha afya kwa kuzingatia alama zote za uandishi.

ZOEZI LA 5.
Soma habari ifuatayo kisha inakili daftarini. Weka alama za uandishi na herufi kubwa kwa usahihi.

Amani anaishi na bibi yake katika kijiji cha Kilole. Anamsaidia bibi yake shughuli za nyumbani. Anamsaidia kusafisha nyumba, kupika, kuosha vyombo na kufua. Juzi Amani alimuliza bibi yake “bibi unajua kusoma” bibi akamjibu ninajua kusoma na kuandika. Amani akasema, sawa bibi kesho kutwa nitaleta kitabu change ili tusome pamoja.

Amani anaishi na bibi yake katika kijiji cha Kilole. Anamsaidia bibi yake shughuli za nyumbani. Anamsaidia kusafisha nyumba, kupika, kuosha vyombo na kufua. Juzi Amani alimuliza bibi yake “bibi unajua kusoma” bibi akamjibu ninajua kusoma na kuandika. Amani akasema, sawa bibi kesho kutwa nitaleta kitabu change ili tusome pamoja.

ZOEZI LA 6. IMLA

Sikiliza kwa makini habari atakayokusomea mwalimu kisha iandike katika daftari.

Imani alimuliza mwendesha baiskeli, “kumetokea nini”? mwendesha baiskeli akamjibu “Nimeteleza na kuanguka chini”. Imani alisikitika sana. akamuliza tena. “Je? Umeumia”? Mwendesha baiskeli akamjibu, Ndiyo. Nimeumia mguu. “Siwezi kusimama.” Imani akauliza

tena "Nikuitie mtu wa kukusaidia?" Mwendesha baiskeli akajibu, Nitashukuru sana msaada wako.

JIULIZE.

Alama ulizojifunza katika sura hii utazitumiaje katika kusoma na kuandika?




Alama nilizojifunza katika sura hii nitazitumia katika kusoma na kuandika kwa kuzifuata na kuzingatia ili niwe nasoma na kuandika vizuri.





Tazama picha zifuatazo kisha soma maelezo yanayohusu picha hizo.

**NDEGE WETU. UK. 83.**

Sifa na tabia za ndege. Kujibu maswali yafuatayo.

1. Taja majina ya ndege unaowafahamu.

| MAELEZO | PICHA |
|---|---|
| Huyu ni kuku. Kuku ni jamii ya ndege. Kuku hutaga mayai na kuangua vifaranga. Mayai ni chakula cha bora. Mimi napenda mayai. |  |
| Mwewe ni ndege. Mwewe huishi juu ya miti. Mara nyingi hupenda kuruka kutokana mti mmoja kwenda mwingine. Mwewe hula vifaranga vya kuku. |  |
| Jogoo ni ndege anayefugwa. Jogoo huwika mapema asubuhi. Watu wengi huamshwa na sauti yake. |  |
| Kasuku ni jamii ya ndege. Ni ndege mwenye rangi nyingi. Anapenda kuiga sauti za binadamu. Mara nyingi hufugwa na binadamu. |  |

| | |
|---|---|
| Huyu ni bata mzinga. Ni jamii ya ndege. Ni ndege anayefugwa. Ni mkubwa kuliko kuku. Ana rangi nyingi sana. Pia hula samaki. |  |
| Huyu ni mbuni. Ni jamii ya ndege. Ni ndege mkubwa wa mbugani. Mbuni awezi kuruka ila ana uwezo wa kukimbia sana. Mbuni hutaga mayai makubwa sana. |  |
| Huyu ni kunguru. Ni jamii ya ndege. Ana rangi nyeusi. Baadhi ya kunguru huwa na doa moja jeupe shingoni. Ndege huyu hula vyakula mbalimbali. |  |
| Huyu ni Chiriku. Ni jamii ya ndege. Chiriku hula nafaka. Ana kelele nyingi. |  |
| Huyu ni bundi, ni jamii ya ndege. Bundi ana macho makubwa. Mara nyingi huonekana usiku. |  |

**Majina ya ndege ninaowafahamu ni**

a) Kuku
b) Kunguru
c) Bata
d) Kasuku

e) Chiriku
f) Bata mzinga
g) Mbuni




2. Ndege hao wanaishi wapi?
   Ndege hao kuna wanaishi porini na kuna wanaoishi nyumbani (wanaofugwa)
3. Ni ndege gani unaowapenda zaidi? Kwa nini?
   Ndege ninaowapenda zaidi ni kuku, bata, bata mzinga. Kwa sababu hutupatia nyama, mayai, manyoya na fedha.

ZOEZI LA 1.


Jibu maswali yafuatayo.


1. Ndege wawili wanaopatikana katika eneo letu ni:
   a) Bata mzinga
   b) Chiriku

2. Kwa kila ndege kueleza rangi yake, ukubwa, anachokula na anayojenga nyumba yake.
   a) Bata mzinga.
      (i) Ana rangi ya nyingi, baadhi ni njano, nyekundu na nyeupe.
      (ii) Ni mkubwa sana
      (iii) Anakula samaki
      (iv) Anajenga nyumba.
   b) Chiriku.
      (i) Ana rangi zaidi ya moja. Njano, nyekundu na nyeusi.
      (ii) Umbo lake ni kubwa kiasi
      (iii) Anakula nafaka
      (iv) Hujenga nyumba kubwa kwa kutumia mitimiti, nyasi na majani kwa kutumia mdomo.
3. Kuchora picha ya ndege watatu na kuandika majina yao

Soma hadithi hii kisha jibu maswali.





URAFIKI WA UWONGO.

Hapo zamani za kale, kulikuwa na kuku na mwewe. Kuku na mwewe walikuwa marafiki sana. Kuku alikuwa na watoto watano na mwewe alikuwa na watoto watatu. Wote walikuwa wanapenda kucheza pamoja. Siku moja kulitokea njaa, mwewe akamwambia kuku waende porini kuwinda. Kuku alikubali na waliwaacha watoto na kuelekea porini. Watoto wa mwewe walikaa juu ya mti na watoto wa kuku walikaa chini ya mti.

Kuku na mwewe walianza safari. Walipokuwa njiani, mwewe alimwambia kuku kuwa amesahau manati yake. Hivyo anarudi kuyachukua. Kumbe mwewe alimdanganya kuku. Mwewe aliaanza safari ya kurudi nyumbani. Kuku alimsubiri mwewe kwa kudhani kuwa atarudi mapema. Kuku alikaa kwa muda mrefu lakini mwewe hakurudi. Kuku aliamua kuanza safari ya kurudi nyumbani. Alipofika alimkuta alimkuta mwewe amekaa juu ya mti na watoto wake. Kuku akamuliza “Rafiki yangu mwewe “watoto wangu wako wapi? Mwewe akamjibu” “Nimewageuza chakula changu” kuku alisikitika sana na kumchukia mwewe. Hadi sasa kuku na mwewe ni maadui.

MASWALI.

1. .......................na .........................................walikuwa marafiki.

   Jibu: kuku na mwewe walikuwa marafiki.

2. Kuku na mwewe walikwenda ..............................................

   Jibu: porini

3. Mwewe alimdanganya kuku ...................................................

   Jibu: kuwa amesahau manati yake hivyo anarudi kuyachukua. Alifanya hivyo kwa sababu aende kula watoto wa kuku.

4. Kilichowatokea watoto wa kuku ni ....................................

   Jibu: kuliwa na mwewe.

5. Kuku alikasirika sana na kumchukia mwewe kwa sababu ...........................................

   Jibu. Alikula vifaranga wake.

6. Hadithi hii inatufundisha.......................................................

   i. Tupendane

   ii. Tusimwamini kila mtu

7. Simulia hadithi hii kwa maneno yako mwenyewe.

Hapo kale kulikuwa na kuku na mwenye. Ndege hawa wawili walipendana sana. Kwani walikuwa wanafanya kazi kwa kushirikiana. Wote wawili walibahatika kupata watoto. Kuku alikuwa na watoto watatu na mwenyewe alikuwa na watoto wawili. Kuku na vifaranga wake walikuwa wanaishi chini ya mti na mwewe alikuwa anaishi juu ya mti. Siku moja kulitokea na shida ya njaa, mwewe akamwambia kuku waende kutafuta chakula. Kuku alikubali wakawaacha watoto wao na kuelekea porini. Njiani mwewe alimwambia kuku kuwa amesahau kuchukuwa manati hivyo anarudi kuyafuata. Mwewe akaanza safari ya kurudi alivyofika nyumbani akawala vifaranga vya kuku na kupanda zake kwenye mti. Kuku alivyochomoka kusubiri na yeye akaamua kurudi, alivyofika hakuwakuta watoto wangu wapo wapi? Mwewe akamjibu, “Nimewageuza chakula change” kuku alikasirika sana na kumchukia mwewe. Hadi leo kuku na mwewe ni maadui wakubwa.

**ZOEZI LA 3.**

<u>Andika Umoja na wingi wa maneno</u>.

| UMOJA | WINGI |
| --- | --- |
| 1. Ndege | Ndege |
| 2. Kiota | Viota |
| 3. Jani | Majani |
| 4. Mti | Miti |
| 5. Mmea | Mimea |
| 6. Mbuni | Mbuni |
| 7. Rafiki | Marafiki |
| 8. Mtoto | Watoto |

ZOEZI LA 4.

Andika ndiyo au hapana.

1. Bata mzinga ni mkubwa kuliko kuku.
   Jibu: ndiyo
2. Njiwa ni mkubwa kuliko kanga.
   Jibu: hapana

3. Kunguru ni mkubwa kuliko mbuni.
   Jibu: hapana

4. Kunguru ana mdomo mfupi kuliko kasuku.

Jibu: hapana

5. Mwewe ni mjanja kuliko kuku.

Jibu: ndiyo
ZOEZI LA 5.

Kamilisha sentensi 1 hadi 6 kwa kutumia maneno yafuatayo.

| |
| --- |
| Ndege Wanyama Mime Matunda Vyombo Vifaa. |

1. Mbuzi, kundoo, ng'ombe na simba ni .......................................
   Jibu: wanyama
2. Kanga, kasuku, kunguru na njiwa ni ....................................
   Jibu: ndege
3. Chungwa, embe, papai, na tikikiti ni ..........................................
   Jibu: matunda
4. Sahani, kikombe, bakuli na kijiko ni ..........................................
   Jibu: vyombo
5. Daftari,chaki, kalamu na kitabu ni ............................................
   Jibu: vifaa
6. Mwembe, mgomba, na machungwa ni ...............................................
   Jibu: mimea.

**JIULIZE.**

Kujifunza kueleza sifa na tabia za ndege kutanisaidiaje katika maisha yangu ya kila siku?.

Jibu: Kujifunza sifa na tabia za ndege katika maisha yangu ya kila siku

kutanisaidia kwamba nikitaka kufuga ndege nitakuwa nimeshajua kila ndege sifa

na tabia zake hivyo nitafuga kulingana na tabia za ndege husika.

**KUANDIKA SENTENSI KWA KUTUMIA NYAKATI.**

Wakati uliopo.
Kutoa taarifa kwa kutumia wakati uliopo.

1. Mama anakwenda sokoni kununua mchele na unga
2. Mwalimu anaandika mazoezi ya Kiswahili ubaoni
3. Shangazi anatumbia nyimbo mzuri
4. Mwanafunzi anasoma kitabu cha hadithi.

**ZOEZI**

**Kubadili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopo.**

1. Mimi na mdogo wangu tukifanya usafi wa mazingira Mimi na mdogo wangu tunafanya usafi wa mazingira
2. Askari walicheza gwaride uwanjani. Askari wanacheza gwaride uwanjani
3. Mjomba aliishi kwenye nyumba ya ghorofa. Mjomba anaishi kwenye nyumba ya ghorofa.
4. Paka alikunywa maziwa. Paka anakunywa maziwa.
5. Kaka alitengeneza kiti. Kaka anatengeneza kiti.

**Wakati ujao.**

**Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.**

1. Mama atapika ugali
2. Shule tutafungua wiki ijayo
3. Shangazi na mjomba watakwenda shambani
4. Bibi atatusimulia hadithi
5. Baba atanunua nyumba

**ZOEZI.**

**Kubadili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati ujao.**

1. Wanajeshi wanaenda vitani. Wanajeshi wataenda vitani.
2. Dada anaenda shule. Dada ataenda shule
3. Mwalimu anafundisha somo la Kiswahili. Mwalimu atafundisha somo la Kiswahili.
4. Mjomba anaishi kwenye nyumba ya ghorofa. Mjomba ataishi kwenye nyumba ya ghorofa.

5. Kaka anatengeneza kiti.. Kaka atatengeneza kit.

**Wakati uliopita. Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.**

1. Kaka alinunua peni
2. Mama alipika wali
3. Rafiki yangu alifua nguo
4. Pasi yetu iliharibika
5. Mwanafunzi alisoma kitabu cha hadithi.

**ZOEZI.**

**Kubadili sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita.**

1. Imani amekula matunda. Imani alikula matunda
2. Binamu yangu amekwenda shambani. Binamu yangu alikwenda shambani
3. Mama amenunua gari. Mama alinunua gari
4. Shangazi na mjomba wamekwenda Arusha. Shangazi na mjomba walikwenda Arusha
5. Paka amekunywa maziwa. Paka alikunywa maziwa.

**Wakati mtimilifu: Soma sentensi hizi kwa sauti.**

1. Mbwa amemg'ata mwizi
2. Embe imeharibika
3. Dada ameandika vizuri
4. Mtoto amelala usingizi
5. Shule imefunguliwa jana.

**ZOEZI.**

**Kubadilisha sentensi hizi ziwe katika wakati mtimilifu.**

1. Mbuzi walilala barabarani. Mbuzi wamelala barabarani
2. Paka alikunywa maziwa. Paka amekunywa maziwa
3. Jagi lilivunjika. Jagi limevunjika
4. Mwanafunzi alisoma kitabu. Mwanafunzi amesoma kitabu
5. Gari liliondoka alfajiri. Gari limeondoka alfajiri.

**SHUGHULI ZA KILA SIKU. Uk 70. Kueleza shughuli zinazofanyika kila siku.**

Kujibu maswali yafuatayo.

1. Huwa unafanya nini kila siku asubuhi? Kila siku asubuhi huwa nafanya:
    a) Natandika kitanda
    b) Ninaoga
    c) Nafanya usafi wa nyumba

d) <u>Ninaoga</u>
e) <u>Najiandaa kwenda shule</u>
f) <u>Naelekea shuleni</u>

2. Taja na eleza shughuli unazofanya kila jumamosi. Shughuli ninazofanya kila jumamosi ni:
   a) <u>Ninaamka napiga mswaki</u>
   b) Nafanya usafi wa nyumba
   c) Nafua nguo
   d) Naoga
   e) Nakunywa chai
   f) Ninaenda kucheza
   g) Ninajisomea

3. Wazazi au walezi wako wanafanya nini kila jumamosi? Wazazi au walezi wangu kila jumamosi wanafanya:
   a) Kusafisha nyumba yote
   b) Wanaoga
   c) Wanakunywa chai

**<u>Kusoma sentensi zifuatazo kwa sauti.</u>**

1. Kila siku asubuhi mama hupika chai.
2. Shangazi husoma kitabu cha hadithi kila siku jioni
3. Kila siku jioni kaka huosha vyombo
4. Mimi husoma kitabu kila siku jioni
5. Mjomba hupenda kuvaa nguo nyekundu kila siku
6. Kila siku bibi hutusimulia hadithi.
7. Dada hufanya mazoezi kila siku asubuhi.
8. Sisi husafisha mazingira ya nyumba ni kwetu kila siku
9. Faraja hupiga mswaki kila sik
10. Mtoto huyu hupenda kulia kila siku.

**<u>ZOEZI LA 1.</u>**

**<u>Tunga sentensi sahihi sita kawa kutumia maneno ya kifungu A, B, na C.</u>**

| KIFUNGU A | KIFUNGU B | KIFUNGU C |
|---|---|---|
| Kila siku mwalimu | Hucheza | Mazoezi ya viungo |
| Kila mara dada | Hufundisha | Wanafunzi darasani |
| Kila jioni kaka | Hufanya | Mpira wa miguu |

**<u>SENTENSI.</u>**

1. Kila siku mwalimu hufundisha wanafunzi darasani
2. Kila mara dada hufanya mazoezi ya viungo
3. Kila jioni kaka hucheza mpira wa miguu
4. Kila siku mwalimu hufanya mazoezi ya viungo
5. Kila jioni kaka hufundisha wanafunzi darasani.


**Soma habari hii.**

Sisi tunaishi katika kujiji cha Dingalo. Hapa kijijini basi huondoka na hurudi kila siku. Basi hilo linaitwa lipayo. Lipanyo huanza safari yake kila siku alfajiri. Likikaribia kituoni hupiga honi kwa nguvu. Wasafiri husubiri basi kituoni. Wale wanaochelewa hukimbia ili kuwahi. Watu hujaa kwenye viti mapema na kisha basi huondoka kuelekea mjini. Basi linapofika mjini, watu hushuka na huendelea na shughuli zao. Dereva hupeleka basi kwenye kituo ha mafuta na hujaza mafuta. Baada ya kujaza mafuta hulirudisha kituoni. Watu wanaokwenda kijijini huanza kupanda kwenye basi. Utingo huingia na kupokea nauli kisha hutoa tiketi.

Ikifika saa nane, Lipango huanza safari ya kurudi kijijini. Hubeba mizigo mingi ya madukanin na mingine ya abiria. Lipayo linapofika karibu na kituo cha kwetu, hupiga honi. Watu wengi huenda barabarani kupokea wageni wao. Wengine huenda kupokea mizigo yao iliyoletwa na basi. Tukifunga shule, mimi na dada tutasafiri na Lipayo kwenda mjini kumsalimia kaka.

**MASWALI.**

1. Basi linalotoka Dingalo huitwa……………….. Jibu: Lipayo
2. Basi hilo husafiri …………….. Jibu: kila siku alfajiri.
3. Lipayo likikaribia kituoni, ……………….. Jibu: hupiga honi
4. Lipayo huondoka mapema sana kijijini kwa sababu …. Jibu: Liwahi kwenda mjini na kurudi kijijini.
5. Kuchora picha ya basi hilo likiwa linasafiri kurudi kijijini.



6. Ndiyo mimi nimewahi kusafiri kwa basi, nilikuwa ninakwenda kijijini kwa bibi njiani niliona miti nyumba za nyasi, wanyama, ndege, na watu wakiuza vitu.

**ZOEZI LA 2**

**Kuandika NDIYO au HAPANA**

1. Lipayo hutoka kijijini mchana …………… Jibu: hapana

2. Basi hubeba mizigo ya maduka tu linaporudi kutoka mjini………………. Jibu: hapana
3. Basi likifika kituoni utingo huwaita wasafiri………………..Jibu: hapana
4. Basi likitoka kijijini linakuwa tupu………………………Jibu. hapana
5. Basi la Lupayo hujaza abiria kila siku……………………..Jibu. ndiyo

**Kutunga habari fupi kuhusu shughuli zinazofanyika kila mara.**

Asha na dada yake wanaishi na bibi yao katika kijiji cha Gezaulole. Hapo hapo kijijini kuna basi ambalo huondoka na kurudi kila siku. Basi hilo huitwa Dungu. Dungu huanza safari yake kila siku asubuhi. Dungu hufika kituo cha basi saa kumi na mbili asubuhi. Dungu hufika kituo cha basi saa kumi na mbili asubuhi na likifika huwwa linapiga honi. Likipiga honi watu hukimbilia na huingia ndani ya gari. Asha na dada yake huenda mjini na kurudi kila siku. Mjini wanaenda kufuata mahitaji yao ya dukani.

**ZOEZI LA 3.**

**Kupanga sentensi hizi kwa mfululizo sahihi ili kupata habari.**

1) Jamali, Hamisi, na Rehema wanasoma darasa la tatu.
2) Hutandika vitabu vyao, huoga na kuvaa sare za shule
3) Hunywa chain na huenda shuleni
4) Husimama mstarini na kuingia darasani
5) Huamka mapema kila siku asubuhi
6) Baada ya masomo hurudi nyumbani
7) Hufagia darasa lao na uwanja wa shule.

**Mfululizo sahihi.**

1. Jamali, Hamisi na Rehema wanasoma darasa la tatu.
2. Huamka mapema kila siku asubuhi.
3. Hutandika vitanda vyao, huoga na kuvaa sare.
4. Hufagia darasa lao na uwanja wa shuleni.
5. Husimama mstarini na kuingia darasani
6. Baada ya masomo hurudi nyumbani

**JIULIZE.**

Kwa nini muhimu kufahamu shughuli za kila siku?

Ni muhimu kufahamu shughuli za kila siku kwa sababu itasaidia kuzifanya kwa muda muafaka.